


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**  
*(Mawasiliano yote yafanywe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)*

**MKOA WA NJOMBE**

**Kumb. WDC/E.30./2/81**



**S. L. P 64,**

**NJOMBE**

**13 Septemba 2019**

**KWA WATUMISHI WA UMMA,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE.**

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA UANDIKISHAJI WA ORODHA YA WAPIGA KURA KATIKA  
UCHAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NGAZI YA VIJJI NA VITONGOJI MWAKA 2019**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 9 (1) na 9 (2) ya Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa mwaka 2019, iliyotolewa kupitia tangazo la serikali Namba 371 la tarehe 26 Aprili 2019 chini ya Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) sura ya 287 zilizotungwa chini ya Kifungu 201A,

Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe anapenda kutangaza nafasi za uandikishaji wa orodha ya wapiga kura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019, kwa kuzingatia Sifa zifuatazo;

1. Awe mtumishi wa Umma anayefanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe
2. Awe mwadilifu na mwaminifu
3. Awe mtu ambaye hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu (Makosa kama wizi, udanganyifu na makosa mengine kama haya)
4. Awe na Umri usiozidi miaka hamsini (50)
5. Asiwe na wadhifa wa Afisa Mtendaji wa Kijiji au Afisa Mtendaji wa Kata
6. Awe anajua kutumia lugha za kiswahili na kiingereza kwa kusoma, kuandika na kunena
7. Awe ni mtumishi wa Umma ambaye anaishi katika eneo ambalo anaomba kufanya shughuli hii ya kuandikisha wapiga kura (Awe mkazi wa kijiji ambacho anaomba kufanya kazi hii)

Maombi yote yalitishwe na Wasimamizi wa Taasisi zenu na yatumwe kwa;

**Msimamizi wa Uchaguzi,  
Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe,  
S.L.P 64,  
NJOMBE**

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya tarehe 17 Septemba 2019 kabla ya saa 9:30 alasiri.

Imetolewa na

Emmanuel R. Kilundo  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**